



# Unachohitaji Kujua Kuhusu Chanjo za COVID-19 kwa Watoto

## 1. Chanjo za COVID-19 zinafundisha miili yetu jinsi ya kupambana na COVID-19 bila kutufanya tuugue.

Chanjo za COVID-19 huipa miili yetu utangulizi mfupi wa jinsi virusi vya COVID-19 vinavyofanya kazi ili mfumo wetu wa kinga uweze kuvitambua na kupambana navyo. Zinafundisha miili yetu jinsi ya kutengeneza protini zinazotokana na ugonjwa mahususi zinazoitwa kingamwili ili kutulinda. Chanjo za COVID-19 hazitupatii COVID-19.

## 2. Utafiti unaonyesha chanjo za COVID-19 ni salama na zenye ufanisi kwa watoto wa umri wa miaka 12-15.

Chanjo zote za COVID-19 zinazopatikana nchini Marekani zilipitia majaribio ya kimatibabu na kuidhinishwa kwa matumizi ya dharura na Mamlaka ya Vyakula na Dawa (FDA) ya Marekani. Zote zimependekezwa na wataalam wa matibabu na afya ya umma kitaifa na hapa katika Vermont.

Majaribio ya kimatibabu ya chanjo ya Pfizer kati ya watoto wa umri wa miaka 12-15 yalionyesha kuwa chanjo ni salama na yenye ufanisi kwa kikundi hicho cha umri. Kati ya watoto waliopata chanjo ya Pfizer wakati wa jaribio la kimatibabu hakuna yeyote aliyepata COVID-19.

Majaribio ya kimatibabu ya chanjo ya Pfizer kati ya watoto wa umri wa miezi 6 yanaanza sasa, na maelezo zaidi yatatolewa hivi karibuni.

## 3. Hatua ya kupata chanjo dhidi ya COVID-19 ina manufaa makubwa kwa watoto wa Vermont.

Kuanzia Mei 2021, zaidi ya watoto 4,000 wa Vermont wametambuliwa kuwa na virusi vya COVID-19 tangu janga lianze, na jambo hili limekuwa na athari kubwa kwa watoto, familia, mipango ya utunzaji wa watoto na shule zetu. Kuwapa watoto wetu chanjo kutawaweka salama na wakiwa na afya na kutasaidia kuzuia kuenea kwa COVID-19 katika jamii zetu.

Kupata chanjo pia kunamaanisha uhuru zaidi ili watoto wa Vermont washiriki shughuli wanazopendelea. Wanaweza kuwatembelea marafiki zao wengine waliopata chanjo bila wasiwasi,

kusafiri ili kutembelea familia nje ya Vermont, na kuepuka hitaji la kujiweka karantini ikiwa watatambuliwa kuwa walitangamana kwa karibu na mtu aliye na COVID-19.

## 4. Chanjo za COVID-19 zilitengenezwa baada ya utafiti wa miongo mingi.

Ingawa virusi vya COVID-19 ni vipya, wanasayansi wamekuwa wakichunguza aina hizi za virusi, vinavyojulikana kama virusi vya korona, kwa miongo kadhaa. Wakati COVID-19 ilipotambuliwa, watafiti ulimwenguni kote walikuwa na lengo moja – kuangamiza virusi hivi vipya vya korona. Jitihada hii ya ulimwengu, pamoja na ufadhili mwingi ulimwenguni kote, zilitusaidia kufikia hatima tukiwa na chanjo salama na zenye ufanisi.

## 5. Watoto wa umri wa miaka 12-15 wanapata athari sawa na vikundi vingine vya umri.

Watoto wa umri wa miaka 12-15 wana athari sawa na watu wazima. Athari za zinazoshuhudiwa sana ni:

- Maumivu kwenye mkono palipodungwa wakati wa kupata chanjo
- Homa
- Kibaridi
- Uchovu

Athari kutokana na chanjo za COVID-19 ni ishara za kawaida kwamba mwili wako unajenga kinga dhidi ya COVID-19. Baadhi ya athari zinaweza kuathiri shughuli za kila siku lakini zinapaswa kuondoka baada ya siku chache. Watu wengine hawapati athari kabisa.

Watu wachache wamepata athari ya mzio kutokana na chanjo, lakini hii ni nadra sana. Ili kuwa salama, kila mtu anayepata chanjo ya COVID-19 anaombwa abaki katika kliniki kwa muda mfupi (kawaida kwa dakika 15) ili aweze kufuatiliwa kwa athari yoyote kali.

## 6. Unaweza kusaidia watoto wako wajihisi kuwa tayari kupata chanjo zao za COVID-19.

Wazazi wanaweza kuchangia pakubwa katika kusaidia watoto kujihisi tayari kupata chanjo yoyote. Unaweza kuzungumza nao kuhusu mambo ya kutarajia wanapopata chanjo, na mambo yanayoweza kutokea katika siku zinazofuata. Wanaweza kujisikia kuumwa kidogo kwa siku moja au mbili baada ya kupata chanjo yao, lakini haitadumu kwa muda mrefu.

Zungumza nao kuhusu jinsi chanjo itafundisha mwili wao kupigana na virusi vya COVID-19, na jinsi hatua ya kupata chanjo inasaidia kulinda kila mtu aliye karibu nao.



## Maelezo zaidi kwa wazazi:

- Kupata Chanjo ya COVID-19 (Idara ya Afya ya Vermont): [www.healthvermont.gov/MyVaccine](http://www.healthvermont.gov/MyVaccine)
- Sayansi Inayotumika katika Chanjo ya COVID-19: Maswali Yanayoulizwa Sana kwa Mzazi (Taasisi ya Wataalamu wa Wototo ya Marekani): [www.healthychildren.org/English/health-issues/conditions/COVID-19/Pages/The-Science-Behind-the-COVID-19-Vaccine-Parent-FAQs.aspx](http://www.healthychildren.org/English/health-issues/conditions/COVID-19/Pages/The-Science-Behind-the-COVID-19-Vaccine-Parent-FAQs.aspx)
- Kuelewa jinsi Chanjo ya COVID-19 Inavyofanya Kazi (Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa): [www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/different-vaccines/how-they-work.html](http://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/vaccines/different-vaccines/how-they-work.html)